


## Ratiba ya maonyesho:

17-18.03.18	Jumamosi	Kuandaa mabanda ya maonesho
19.03.18	Jumatatu	Kumalizia maandalizi
20-21.03.18	J4 & J5	Siku 1 & 2 za maonesho
22-23.03.18	Alhamisi	Kuondoa mabanda na kufuatilia wateja husika

Mawasiliano na namna ya kufika eneo la maonesho  
Kituo cha Mafunzo ya Viwanda vya misitu, Mafinga (KMVVM)  
Kinyanambo, Mafinga

Tukuswiga Ikasu Tel:+255 7554633173 or David Msuya Tel+255756997500

Uelekeo: Kutoka kituo cha mafuta cha CF, njia panda madibira, endesha 2.5km, fuata kibao cha kituo kitakachokuwa kushoto mkabala na kiwanda cha kutengenza mkaa mwendo wa wastani wa nusu kilomita utakuwa umefika, tazama ramani hii



## MAONYESHO YA KIBIASHARA YA VIWANDA VYA MAZAO YA MISITU NA MBAO NYANDA ZA JUU KUSINI



## KITUO CHA MAFUNZO YA VIVANDA VYA MAZAO YA MISITU NA MBAO, MAFINGA, IRINGA

**TAREHE 20 - 21 MACHI 2018**

## Ni nini?

Maonesho ya kibiashara ya KVVMM yana lengo la kuwaleta pamoja washiriki wote kutoka sekta ya misitu na viwanda vya mbao, kuanzia wale wakulima binafsi wa miti, viwanda vya mbao pamoja na wazalishaji mitambo katika tukio litakalo wakutanisha. Lengo la tukio hili ni kuwakutanisha wauzaji na wanunuzi wanaokidhi viwango katika sekta hii.

## Ni siku gani?

Ni tarehe 20-21 ya mwezi machi, 2018

## Ni kwanini ushiriki manonesho?

Maonesho ya KVVMM ndio ya kwanza na makubwa kuwahi kufanyika nchini Tanzania katika sekta hii yatakatotoa fursa kwa wadau kuonesha bidhaa na huduma zao za kisasa kabisa, kukukutanisha na wadau katika sekta pamoja na wateja. Usikose, weka sasa nafasi yako ya ushiriki usio na gharama yoyoyte.

Wakulima wa miti wadogo na wakati mnaamasishwa kushiriki kwa wingi.

Ushiriki wa maonesho haya ni bure kabisa. Programu itatoa nafasi kwa utaratibu wa kumhudumia yule anaetangulia kufika. Washiriki wanakaribishwa kutembelea maeneo yatakayowekwa vibanda vya maonesho ili kujua utaratibu utakaotolewa na wafanyakazi wa programu.



## Makundi ya maonesho:

- A. Huduma za kituo cha mafunzo ya viwanda vya misitu na mbao
- B. Vyama vya wakulima wa miti na viwanda vya mbao
- C. Huduma za kifedha kwa wakulima wa miti na wachakata mbao
- D. Dhana na vifaa mahususi kwa bustani za miche
- E. Vifaa vya uvunaji wa mazao ya misitu na usafirishaji wa magogo
- F. Vifaa vya uchanaji na uchakataji mbao mahususi kwa viwanda vidogo vidogo na vya kati.
- G. Vifaa vya kukaushia na kuhifadhi mbao.
- H. Upatikanaji wa kudumu wa mbao zinazotoka kweye mashamba ya miti nchini:
  - a. Vibebeo/vifungashio
  - b. Mbao
  - c. Bodi/mbao za kutengenezea paneli
  - d. Viwanda vidogo vidogo vya kuchakata mbao na kutengeneza samani
  - e. Mbao za ujenzi
- I. Vifaa mahususi kwa utengenezaji wa mkaa
- J. Usambazaji wa umeme vijijini kwa ajili ya maendeleo ya viwanda
- K. Nguzo za usambazaji umeme